SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 2 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I2.1353

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Kushamiri Kwa Dhamira Ya Mapenzi Katika Muziki Wa Bongofleva: Dalili Za Kudumaa Kwa Sanaa

Mohamed Yonis Khalifa

Department of Languages and African Studies, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Mabenzi
Mbalimbali
Katika
Kuwa
kazi

**ABSTRACT**

Sanaa ni taaluma pana inayojumuisha tanzu mbalimbali lakini malengo ya tanzu hizi hufanana. Mfano; muziki, filamu, ushairi, uchoraji, na uchongaji ni miongoni mwa tanzu mbalimbali za sanaa zinazotofautiana kimuundo lakini zote hulenga aidha katika kuelimisha, kuburudisha, ama kudumisha utamaduni wa jamii husika. Makala hii inachunguza kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika sanaa ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania maarufu kama Bongofleva. Ni dhahiri kuwa kazi moja ya fasihi inaweza kubeba zaidi ya dhamira moja katika maudhui yake kulingana na mambo mahususi yanayojadiliwa katika kazi hiyo. Katika zama za hivi karibuni, muziki wa kizazi kipya wa Bongofleva umekuwa ukitawaliwa na dhamira ya mapenzi pekee kwani wasanii wengi wamekuwa wakirekodi nyimbo zilizosheheni kwa asilimia kubwa maudhui ya kimapenzi. Aidha, neno ‘mapenzi’ katika makala hii linamaanisha mahusiano ya kimapenzi baina ya mwanaume na mwanamke

# دراسة في تطوير الموسيقى:((بونقوفليفا))دراسات من المقالات الأدبية

محمد يونس خليفة

قسم اللغات الأفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
المحبة
مختلفة
في
يكون
العمل

**الملخص**

الفن مجال واسع يتألف من أقسام فرعية مختلفة ولكن أهداف هذه التقسيمات الفرعية متشابهة. مثال: تعدد الموسيقى والأفلام والشعر والرسم والنحت من بين فروع الفن المختلفة، التي تختلف في البنية ولكنها تركز جميعها إما على التعليم أو الترفيه أو الحفاظ على ثقافة المجتمع المعني. يستكشف هذا المقال العاطفة المزدهرة للشغف بفن موسيقى الجيل الجديد في تنزانيا المعروف شعبياً باسم Bongofleva. من الواضح أن العمل الأدبي الواحد يمكن أن يحمل أكثر من موضوع واحد في محتواه اعتمادًا على التفاصيل التي تمت مناقشتها في هذا العمل. في الآونة الأخيرة ، سيطرت النوايا الرومانسية على الجيل الجديد من الموسيقى في Bongofleva حيث قام العديد من الفنانين بتسجيل الأغاني التي تحتوي على نسبة عالية من المحتوى الرومانسي. علاوة على ذلك ، فإن كلمة "حب" في هذه المقالة تشير إلى العلاقة الرومانسية بين الرجل والمرأة.

## Muziki wa Bongofleva

Kwa kifupi, bongofleva ni muziki wa kizazi kipya unaoimbwa nchini Tanzania. Neno bongofleva ni muunganiko wa maneno mawili yaani *bongo* na *fleva*. *Bongo* ni neno la kiswahili lililotokana na neno *ubongo*. Kutokana na madai ya vijana na watu wengi kwamba kuishi katika jiji la Dar es Salaam kunahitaji akili sana, watu walilibatiza jiji hilo jina la *bongo* na badae neno hilo likajipatia umaarufu na hivyo vijana wengi walianza kutumia neno hilo kumaanisha jiji la Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla (Sanga, 2011). Kwa upande mwingine, neno *fleva* ni nominomkopo iliyotokana na neno *flavor* kutoka katika lugha ya Kiingereza. Katika lugha ya kiswahili, neno *fleva* linaweza kutafsiriwa kama *ladha*, hivyo *bongofleva* maana yake ni *ladha ya bongo*. Sifa kubwa ya muziki wa bongofleva ni ladha ya kitanzania inayochanganywa na misimu, mistari ya Kiswahili inayochanganywa na maneno ya lugha za kigeni kama vile Kiingereza,Kifaransa na lugha zingine. Sifa hii inaonesha dhahiri kuwa vijana ndio wanaojihusisha sana na muziki huu na ndio maana muziki wenyewe unaitwa *muziki wa kizazi kipya*. Vilevile, mziki wa bongofleva ni mchanganyiko wa tanzu mbalimbali za mziki kutoka

*Corresponding author:
E-mail addresses: moh.abouqrasah@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 11 July 2021 - Received in revised form 23 October 2021 - Accepted 28 October 2021*

mataifa mengine kama vile Zouk, R&B, Raggae na muziki wa kufoka, yaani Rap (Suriano, 2007). Baadhi ya wataalamu kama vile (Chachage, 2002; Mangesho, 2003) wanadai kuwa muziki wa bongofleva uliingia nchini Tanzania miaka ya 1980 hadi 1990 na ukaanza kujipatia umaarufu kwa jina la hiphop na mwishowe ulijizolea mashabiki na wapenzi kutoka kwenye kundi la vijana. Bongofleva ni muziki endelevu na unakua kila siku kama Omari (2006) na Jilala (2008) wanavyoeleza juu ya bongofleva kama fasihi pendwa ambayo inakua kilasiku na kupata wafuasi wengi.

**Dhamira ya Mapenzi katika Muziki wa Bongofleva**

Kama kazi zingine za sanaa, muziki unaweza kuzungumzia dhamira mbalimbali kama vile uchumi, siasa, utamaduni, jamii, imani na dhamira nyingine nyingi. Kazi ya sanaa inapoangazia dhamira fulani, huiathiri hadhira moja kwa moja kutokana na jumbe zilizobebwa kwenye maudhui ya kazi husika. Makala hii itaangalia nyimbo za wasanii mbalimbali wa muziki wa bongofleva kuona jinsi dhamira ya mapenzi ilivyoshamiri katika kazi hizo. Ni dhahiri kuwa wasanii wengi wa muziki wa bongofleva wamekuwa wakiegemea kwenye dhamira ya mapenzi katika kazi zao. Mapinduzi haya katika muziki wa kizazi kipya yametokana na utandawazi uliokuja baada ya tamaduni za mataifa mbalimbali kuanza kuingiliana kupitia vyombo vya habari na mitandao mingine. Dhamira ya mapenzi katika nyimbo za bongofleva imekuwa ikisawiriwa katika namna kuu mbili, yaani namna ya kwanza ni pale msanii anapomsifu mpenzi wake kupitia tungo za muziki na namna ya pili ni pale msanii anapokuwa anaeleza hisia za kuteseka na huba zinazotokana na kuumizwa na mpenzi wake. Maelezo yafuatayo yanaelezea namna dhamira ya mapenzi inavyosawiriwa katika muziki wa bongofleva.

**Nyimbo za Kumsifu Mpenzi**

Wasanii wa bongofleva wamekuwa wakiandika tungo zenye ujumbe wa kumsifu mpenzi na nyimbo hizi zimekuwa zikipokelewa vizuri na hadhira kwasababu asilimia kubwa ya vijana wapo katika mapenzi na wanafurahia zaidi wanaposikiliza nyimbo zenye maudhui ya kusifu mapenzi pengine kwa sababu za kuboresha mahusiano yao au kuburudika. Watu waliopo kwenye huba zito hupokea nyimbo za kusifu wapenzi kwa furaha kwani wengi huburudishwa na nyimbo za namna hii hususani wanapokuwa na wenzi wao. Makala hii imetumia nyimbo tatu za wasanii maarufu nchini Tanzania zenye ujumbe wa kusifu mpenzi kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

| *Baikoko -Mbosso Ft Diamond Platnumz* | *Kiuno- Rayvanny* | *Dodo –Ali Kiba* |
|---|---|---|
| *Ayo Laizer...* | ***Baby baby ayi ayi ayi*** | ***Yeah (Ye Baba)*** |
| *Kako fine kila nikikaeka kwenye Line, bilabila* | ***Michepuko ya zamani bye bye bye*** | ***Kupenda ni vitendo*** |
| *Shuwaini, kwake nimelewa kama wine tilalila.* | ***Mi najidai dai dai, oh we subiri shera dai dai dai*** | ***Si maneno maneno*** |
| *Ye sisimizi nami Gegedu tuna Gegeduana.* | ***Zungusha pepeta ungo, nipe mambo yakizania*** | ***Leo nakupa kitengo*** |
| *Nilivyo sina jinsi Tajiri wa Mbegu namuhonga na* | ***mafumbo*** | ***Kwa kufika malengo*** |
| *Mwana* | ***Geuka onyesha umbo, jiachie wala usibane*** | ***Umeziba mapengo*** |
| *Baba Mndenge Mama Mzaramo uno lake la* | ***tumbo*** | ***Kwa upendo upendo*** |
| *kurithi* | ***You're forever be my always aya yeh*** | ***Eeh bwana wala huzingui*** |
| *Kafunga tenge mwari chakalamu shetani mwana* | ***Cake of my birthday aya ye*** | ***Anzeni vikao vya send off yeah*** |
| *ibilisi* | ***Director of my always, baby you turn Thursday*** | ***Maana we mrembo nakujuza*** |
| *Jipuu, uchungu mwana nyuma umejaza* | ***to be holiday*** | ***Mama nashukuru umekuza*** |
| *kishundundu* | ***We ndio kiboko wa chunusi na harara, we zaidi*** | ***Chanda chema pete nitakutunza*** |
| *Kwenye zipu Kuna kirungu usikamate utawaita* | ***yao (hao)*** | ***Nambaa moja wote waburuza*** |
| *wazungu* | ***Sura yako hata ukitoka kulala bado zaidi yao*** | ***Na umeshanizima*** |
| *Eeh Heeh...* | ***Basi kata taratibu (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Babu mkuna nazi Aah Haah achutama kishinani* | ***Kiuno cha pakashungu (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Na msuli wake uko wazi mambo yote Hadharani* | ***Pangaboy feni bovu (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Go! Go! Go! Go! Goal.* | ***We pinda mpaka mugongo (kiuno)*** | ***Your love your love*** |
| *Mtoto anadaka Goli kipa Runyamira)* | ***Nipe uno la uzazi (kiuno)*** | ***Na umeshanizima wee*** |
| *Wabeja* | ***Mpaka chini kwa udongo (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Tena akikata anaitikisa sababu* | ***Basi kati- katika (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Baby acha unachezaga* | ***Kama unatokea kongo (kiuno)*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *(Baikoko)* | ***Kanitesa Suzy eh, kanitesa Monica*** | ***Your love your love*** |
| *Unavyo baby* | ***Kanitesa Shuvele, kanitesa Wini eh*** | ***Ka majani na udongo yeah*** |
| *(Baikoko)* | ***Ila si wewe wewe wewe mama mama*** | ***Nnje ya sayari nikuite kimondo oooh*** |
| *Unavyoinyonga aah* | ***Mhh shivonipele*** | ***Kama chungu ya kibongo*** |
| *(Baikoko)* | ***Yawawili mapenzi oh, watatu siwezi oh*** | ***Na usiyape time yakutibue nyongo (No)*** |
| *Eeh waonyeshe* | ***Usisikie maneno maneno maporojo*** | ***Maana we mrembo nakujuza*** |
| *(Baikoko)* | ***watakuumiza roho roho oh*** | ***Maana nashukuru umekuza*** |
| *Baby acha unachezaga* | ***Yawawili mapenzi oh, watatu siwezi oh*** | ***Chanda chema pete nitakutunza*** |
| *(Baikoko)* | ***Usisikie maneno maneno maporojo*** | ***Nambaa moja wote waburuza*** |
| *Unavyo baby* | ***watakuumiza roho roho oh*** | ***Na umeshanizima eh*** |
| *(Baikoko)* | ***Maliza eh maliza eh, mama nipe yote*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Unavyoinyonga aah* | ***Taamu nipe yote yote*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *(Baikoko)* | ***Maliza eh maliza eh maliza eh ah*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Eeh waonyeshe* | ***You're forever be my always aya yeh*** | ***Your love your love*** |
| *(Baikoko)* | ***Cake of my birthday aya ye*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Asa komesha dengua* | ***Director of my always, baby you turn Thursday*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Dengua baby dengua* | ***to be holiday*** | ***Na yoyoyoyoyo-your love*** |
| *Ringa Dengua! Dengua* | ***We ndio kiboko wa chunusi na harara, we zaidi*** | ***Your love your love*** |
| *Deka Dengua! Dengua wakuone* | ***yao (hao)*** | ***Dodo, mama dodo (Dodo langu wewe)*** |
| *Kanivua ndala miguu anataka nipite peku* | ***Sura yako hata ukitoka kulala bado zaidi yao*** | ***Dodo, mama dodo (Hata utikisa halitodondoka)*** |
| *Pekupeku….* | ***Basi kata taratibu (kiuno)*** | ***Dodo, mama dodo (Dodo langu wewe)*** |
| *Kunduchi juu anifikishe kwetu* | ***Kiuno cha pakashungu (kiuno)*** | ***Dodo, mama dodo (Dodo)*** |
| *Embu tamu Ladha ya kitumbua* | ***Pangaboy feni bovu (kiuno)*** | ***Dodo, dodo langu wewe*** |
| *Rojo ya Embe Kibada! Kibadah* | ***We pinda mpaka mugongo (kiuno)*** | ***Dodo, dodo, dodo langu wewe*** |
| *Hodari kunengua miuno ya ushubwada!* | ***Nipe uno la uzazi (kiuno)*** | ***Hata utikisa halitodondoka*** |
| *Shubwadah* | ***Mpaka chini kwa udongo (kiuno)*** | ***Mama muogopa, mama muogopa..*** |
| *Nyuma kalisasambua kafungasha midabwada!* | ***Basi kati- katika (kiuno)*** | ***Mama muogopa, mama muogopa.*** |
| *Bwaadah* | ***Kama unatokea kongo (kiuno)*** | |
| *Anavyo tafuna mua ka kibogoyo Dada!* | ***Tupate moja moto moja baridi (cheza cheza bila*** | |
| *Katoto kamelainika kwala* | ***kutoka jasho)*** | |
| *Kukapa Ndizi Banana* | ***Nyama choma supu ya digi digi (cheza cheza bila*** | |
| *Nakapeleka kwa Mama! Mama Mama Dangote* | ***kutoka jasho)*** | |
| *Kama kuku twakimbizana! Zana* | ***Kibosi bosi kipedeshee (cheza cheza bila kutoka*** | |
| *Kana ibuka Kana zama* | ***jasho)*** | |

| | | |
|---|---|---|
| *Kamwili kana balaa na Lana! Laana Laana kazote.* | ***Tumia pesa ikuzoee (cheza cheza bila kutoka jasho)*** | |
| *Ebooh!* | | |
| *Mtoto anadaka Goli kipa Runyamira)* | | |
| *Wabeja* | | |
| *Tena akikata anaitikisa sababu* | | |
| *Baby acha unachezaga* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Unavyo baby* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Unavyoinyonga aah* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Eeh waonyeshe* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Baby acha unachezaga* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Unavyo baby* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Unavyoinyonga aah* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Eeh waonyeshe* | | |
| *(Baikoko)* | | |
| *Asa komesha dengua! Dengua* | | |
| *Baby dengua! Dengua* | | |
| *Ringa Dengua! Dengua* | | |
| *Deka Dengua! Dengua wakuone* | | |
| *Kama anaifata, Anainama Anainuka mwari Anaisusa* | | |
| *Kwakujishebedua, Anainama Anainuka mwari anaisusa* | | |
| *Kama Hataki mwari* | | |
| *Anaima Anainuka mwari Anaisusa* | | |
| *Kwa madoidoi* | | |
| *Anaima Anainuka mwari Anaisusa* | | |

**Nyimbo zinazosawiri Kuteseka na Huba**

Nyimbo hizi zinaimbwa kusawiri usaliti wa mapenzi unaotokea baina ya watu wawili walio kwenye mahusiano ya kimapenzi. Ujumbe unaobebwa katika nyimbo hizi unaweza kuashiria vijembe baina ya wapenzi walioachana au malalamiko ya mmoja wa wapenzi walioachana kutokana na maumivu makali ya huba yanaoutesa mtima wake. Wakati mwingine, nyimbo hizi zinaweza zisibebe ujumbe uliojaa vijembe badala yake zinabeba ujumbe unaomuonesha mmoja kati ya wapenzi wawili akibembeleza huba kwa mwenzi wake ambae hawana mahusiano mazuri katika nyakati fulani. Jedwali lifuatalo linaonesha nyimbo tatu za bongofleva zenye maudhui ya lawama za huba zilizoimbwa na wasanii maarufu wa bongofleva.

| *Infidèle – Alikiba* | *Ex Boyfriend - Rayvanny* | *Tuachane - Lavalava* |
|---|---|---|
| *Ilibidi tu nijiongeze* | ***Leo nakula kwa macho*** | ***Kama imeshindikana kunirudia isiwe tabu*** |
| *Niliisha* | ***Nguvu ya kusema sina*** | ***Usiuforce moyo kupenda usipo stahili*** |
| *Pia bora nijipongeze* | ***Maneno ya mipasho*** | ***Ya Nini Kung'ang'ania nishachoka kuwekwa*** |
| *Naona yame kwisha* | ***Na jeuri vimeshazima*** | ***sub*** |
| *Akili uliniweza maskini* | ***Nilishafuta namba zako*** | ***Siwezi oh na mapenzi nishaghaili*** |
| *Uliniweza mie ukanijua* | ***Nikachoma picha zako*** | |
| *Nilipungua sana bwana* | ***Sikujali ulivyolia*** | ***Tena niko tayari*** |
| *Ila tu unanicheka* | ***Mbele ya mashoga zako*** | ***Vipigwe vinumbi kengere kwa sherehe*** |
| *Ukatawala moyo* | ***Nikasema uende zako*** | ***Kinaga ubagha*** |
| *Ukachukua bila aibu ukanitesa versuri.online…* | ***Nguo nikakutupia*** | ***Mbele ya umati tuachane*** |
| *Kumbe ni liar unaweza niacha me niuliwe* | ***Na zaidi uliuguza vindonda*** | ***Na kama hautojali*** |
| *Na mabwana zako wewee* | ***Kwa vipigo manyanyaso kila siku*** | ***Tuite waumini mapadri na masheikh*** |
| *Kumbe ni liar unaweza niacha me niuliwe* | ***Kwa mawazo ukakonda Niko bussy kuchiti*** | ***Yaishe labda sa kwa nini tutesane*** |
| *Na mabwana zako ooohh* | ***Nafungua zipu*** | |
| *Bora nikuache we uende, nami niende* | ***Ulinibembeleza nikakubeza*** | ***Kweli we ndo nikupendae*** |
| *Tusiishi kizembe, niache mawenge* | ***Unanuka na nikatukelekeza*** | ***Ila unanipa ghadabu jina*** |
| *Bora uende, nami niende* | ***Macho makengeza miguu ya pweza*** | ***Tusitoane nyongo*** |
| *Tusiishi kizembe, niache mawenge ah ah* | ***Kuwa nawe nkasema niliteleza*** | ***Na kama umenichoka eh*** |
| *Donc, j'ai finalment* | ***Leo unapendeza wamekutengeneza*** | ***Niache ki staarabu jina*** |
| *Repris mes esprits* | ***Wanaume wenye mali wenye fedha*** | ***Usinipe chongo iye*** |
| *Parce que j'étais perdu* | ***Sasa unajiweza na siwezi kujikweza*** | |
| *Parce que j'étais perdu* | ***Najutia nafasi kuipoteza*** | ***Mwili umebaki kongoro*** |
| *Et je dois me féliciter pour réussir* | ***Leo aibu yangu*** | ***Nyama sina ni mifupa*** |
| *Tu me connaissais* | ***Ex boyfriend*** | ***Naiona ndomboro*** |
| *Si bien donc tu m'avais* | ***Ex boyfriend*** | ***Kabisa siwezi furukuta*** |
| *Dans le creux de la main* | ***Ex boyfriend*** | ***Penzi kiporo*** |
| *Dans le creux de la main* | ***Siiti tena honey baby jina langu limekua*** | ***limeshachina linanuka*** |
| *J'étais en mal point alors* | ***Ex boyfriend*** | ***Huishi kokoro*** |
| *J'ai maigri mais tu t'en fiches* | ***Ex boyfriend*** | ***Purukushani kutwa kucha iyeeh*** |
| *Kumbe ni liar unaweza niacha me niuliwe* | ***Ex boyfriend*** | |
| *Na mabwana zako wewee* | ***Sikujua kumbe tabu peke yangu naugua*** | ***Bora tuachane*** |
| *Kumbe ni liar unaweza niacha me niuliwe* | ***Nawaza nilifeli wapi kusema sikutaki*** | ***Bora tuachane siwezi*** |
| *Na mabwana zako ooohh* | ***Sura ya baba na kitambi cha makapi*** | ***Bora tuachane*** |
| *Bora nikuache we uende, nami niende* | ***Sasa unamtanashati bitozi tena smart*** | ***Yamenishinda mapenzi*** |
| *Nisiishi kizembe, niache mawenge* | ***Mtu wa gym tena ana six-pack*** | ***Mi naona bora tuachane eeh*** |

*Bora uende, nami niende*
*Nisiishi kizembe, niache mawenge ah ah…*

***Mi nipo juu ya bati***
***Sina mikakati***
***Ghetto mwendo chai na chapati***
***We ushahama mburahati***
***Una nyumba masaki***
***Mnachoma nyama kila siku party***
***Ushanipiga mikuki aah***
***Insta mi sifurukuti aah***
***Mambo ya gauni suti aah***
***Mkifanya photoshoot aah***
***Mapenzi hayana commando***
***Mwenzako unaniuma roho***
***Natamani nikuite njoo***
***Turudi kama before***
***Kumbe shape ilijificha kwenye dera***
***Hizo skin-jeans mama zinakera***
***Utaniletea kadi kwenye machela***
***Siku wakikuvalisha shela***
***Na ulinibembeleza nikakubeza***
***Unanuka na nikakutelekeza***
***Macho makengeza miguu ya pweza***
***Kuwa nawe nkasema niliteleza***
***Leo unapendeza wamekutengeneza***
***Wanaume wenye mali wenye fedha***
***Sasa unajiweza na sio najikweza***
***Najutia nafasi kuipoteza***
***Leo aibu yangu***
***Ex boyfriend***
***Ex boyfriend***
***Ex boyfriend***
***Siiti tena honey baby jina langu limekua***
***Ex boyfriend***
***Ex boyfriend***
***Sikujua kumbe tabu peke yangu naugua***

***Tuachane siwezi***
***Bora tuachane***
***Yamenishinda mapenzi***

***Ni dhahili Kisima kimekauka maji***
***Ndo maana naona kata sina maana tena***
***Nilifikiri mi gonjwa langu limepata mponyaji***
***Umeniongezea homa mwili wote wantetema***

***Mi naona basi***
***Labda si riziki yangu***
***Kama hunitaki***
***Acha tu niende zangu***
***Ya nini mishikaki***
***Ntatafuta boda yangu***
***Nijinafasi***
***Niipande peke yangu***

***Mwili umebaki kongoro***
***Nyama sina ni mifupa***
***Naiona ndomboro***
***Kabisa siwezi furukuta***
***Penzi kiporo***
***limeshachina linanuka***
***Huishi kokoro***
***Purukushani kutwa kucha iyeeh***

***Bora tuachane***
***Bora tuachane, siwezi***
***Bora tuachane***
***Yamenishinda mapenzi***
***Mi naona bora tuachane eeh***
***Tuachane siwezi***
***Bora tuachane***
***Yamenishinda mapenzi***

***Ooh oh! Liwalo na liwe***
***Na namba zako ntafuta ama unasemaje***
***Limalo na liwe nguo zako mashuka***
***Wacha nkazimwage***
***Liwalo na liwe***
***Sio kama nimesusa***
***Ila ntafanyaje ?***
***Liwalo na liwe we kaa mi nanyanyka***
***Acha tu niagee***
***Hiiiiii…***

**Sababu ya Kushamiri kwa Dhamira ya Mapenzi katika Muziki wa Bongofleva**

Kwanini dhamira ya mapenzi ishamiri hasa katika muziki wa bongofleva katika zama za sasa? Zinaweza kuwepo sababu nyingi zinazosababisha kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika mziki wa bongofleva, lakini sababu kubwa ni kukua kwa soko la muziki huo.

**Soko la Muziki**

Kwa asilimia kubwa, vijana hutumia muda mwingi sana wakifikiri au wakizungumza juu ya wao kuwa katika mahusiano ya kimapenzi (Furman 2002). Tabia hii huwafanya kuwa wateja wa nyimbo ambazo zinagusa kwa namna moja au nyingine mahusiano yao ya kimapenzi. Nchini Tanzania, vijana wengi ndio wamekuwa soko kubwa la muziki wa bongoflava kutokana na wao kufurahishwa zaidi na nyimbo zenye dhamira ya mapenzi ukilinganisha na dhamira zingine kama siasa, uchumi na mambo mengine ya kijamii. Hivyo basi, wasanii wengi wa kizazi kipya nchini Tanzania huangalia soko la muziki kabla hawajarekodi nyimbo zao. Kwa kifupi, nchini Tanzania wasanii wengi wa bongofleva wanaosawiri dhamira ya mapenzi katika nyimbo zao hupata wateja wengi sana katika mitandao ya kijamii ukilinganisha na wasanii wachache wa bongofleva wanaosawiri dhamira nyingine tofauti na mapenzi. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya watazamaji na wasikilizaji wa nyimbo zenye dhamira ya mapenzi dhidi ya nyimbo zenye dhamira ya siasa katika mtandao maarufu wa YouTube.

| Wimbo | Msanii | Dhamira Kuu | Kuchapishwa | Watazamaji YouTube |
|---|---|---|---|---|
| Tuachane | Lavalava | Mapenzi | 2018 | Zaidi Ya Milioni 14 |
| Kiuno | Rayvanny | Mapenzi | 2021 | Zaidi Ya Milioni 5.8 |
| Baikoko | Mbosso | Mapenzi | 2021 | Milioni 10 |
| Zimbabwe | Roma | Siasa | 2018 | Milioni 3 |
| Nchi ya ahadi | Kala Jeremiah | Siasa | 2015 | Zaidi ya Milioni 1 |
| Waite | Mrisho Mpoto | Siasa | 2015 | Laki 4 na elfu 97 |

**Chanzo:YouTube**

Jedwali hili linaonesha idadi ya watazamaji na wasikilizaji wa nyimbo zinazosawiri dhamira ya mapenzi katika mtandao wa YouTube dhidi ya nyimbo zinazosawiri dhamira ya siasa. Nyimbo zinazosawiri dhamira ya siasa zimeoneshwa kuwa na watazamaji wachache katika mtandao wa YouTube licha ya kuwepo katika mtandao huo kwa muda mrefu ukilinganisha na nyimbo zinazosawiri dhamira ya mapenzi. Hii inathibitisha kuwa wasanii wengi wanarekodi nyimbo zenye dhamira ya mapenzi ili kuendana na mahitaji ya soko la muziki kwani kinyume na hivyo, watapata mauzo hafifu.

**Utandawazi**

Utandawazi ni mchakato wa kuunganisha siasa, tamaduni,na chumi za nchi mbalimbali pasipo kuweka vikwazo vya kimuingiliano. Kwa mujibu wa Jesseemurithii (2018), Utandawazi unahimiza sana uondoaji wa vikwazo vya kibiashara baina ya mataifa mbalimbali na kuifanya dunia kuwa soko moja lisilo na mipaka, unahimiza soko huria, demokrasia katika siasa za mataifa yote, utawala bora na uzingatiwaji wa haki za binadamu. Muingiliano huu unasababishwa na maendeleo ya kiteknolojia hasa katika tasnia ya habari ambayo kupitia televisheni pamoja na mitandao mbalimbali, watu wamekuwa wakiwasiliana na kupelekea muingiliano mkubwa wa kiutamaduni. Utandawazi umechangia kwa kiasi kikubwa kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika muziki wa bongofleva kwani wasanii wa bongofleva wamekuwa wakiimba maudhui yanayoimbwa katika mataifa kama Marekani na mengine ya Ulaya. Ushahidi unaonekana katika video za nyimbo za wasanii wengi wa bongofleva ambazo zinajumuisha watu wenye mavazi yanayoonesha maungo ya siri kitu ambacho si utamaduni wa kitanzania na Afrika kwa ujumla bali ni utamaduni wa Ulaya, Marekani na baadhi ya nchi za Asia.

**Kushuka kwa Ubunifu**

Ubunifu ni kiungo muhimu sana katika kazi yoyote ya sanaa kwani bila ubunifu, kazi za sanaa hazitokuwa na mvuto kwa jamii. Ubunifu ni kitendo cha kutumia ufundi na ujuzi katika kuboresha kitu fulani. Kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika muziki wa bongofleva kunaonesha dhahiri kuwa ubunifu miongoni mwa sanii unashuka na kwamba wengi wamekuwa wakiwaiga wasanii wengi ambao wanafanya vizuri katika muziki wenye dhamira ya mapenzi. Baadhi ya wasanii wa bongofleva wamekuwa wakijitahidi kuwa wabunifu katika muziki wao na hivyo kujikuta wanafanya vizuri katika soko licha ya kuwa wameimba juu ya dhamira zingine tofauti na mapenzi. Mfano mzuri wa wasanii ambao wanaimba juu ya dhamira ya siasa kwa ubunifu wa hali ya juu ni Roma pamoja na Stamina ambao kwa pamoja wanaunda kikundi maarufu cha muziki wa bongofleva kinachojulikana kwa jina la ROSTAM. Hivi karibuni, ROSTAM wamerekodi wimbo unaoitwa 'hujambo mwanangu?' wenye maudhui ya kisiasa na tayari wimbo huo unafanya vizuri katika mitandao. Hivyo basi, kushuka kwa ubunifu kunafanya wasanii wengi wajikite katika kuimba juu ya dhamira ya mapenzi pekee wakidhani kuwa soko linahitaji muziki wa kimapenzi pekee.

**Je, Sanaa Inadumaa Nchini Tanzania?**

Kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika nyimbo za bongofleva hakujasababisha kudumaa kwa sanaa nchini Tanzania. Baadhi ya wasanii wamekuwa wakirekodi nyimbo zenye dhamira tofauti na mapenzi kama vile siasa na utamaduni wa nchi ya Tanzania licha ya kuwa muziki wao haufanyi vizuri sana katika soko kwani soko linahitaji zaidi dhamira ya mapenzi katika nyimbo za bongofleva. Hata hivyo, kushamiri kwa dhamira ya mapenzi katika muziki wa bongofleva kunaathiri kwa namna moja ama nyingine misingi ya maadili ya vijana kwani wanajikita katika kusikiliza nyimbo za mapenzi pekee badala ya kujikita katika dhamira nyingine tofauti zinazoweza kuleta mchango chanya katika jamii kama vile ukombozi wa kiuchumi, kisiasa, kijamii pamoja na maadili mema. Soko linaweza kuwa linawataka wasanii kuimba dhamira za mapenzi lakini ni dhahiri kwamba kama wasanii watakuwa wabunifu katika nyanja zingine za kijamii, siasa, na uchumi basi wanaweza kufanya mageuzi ya soko la muziki.

**Hitimisho**

Makala hii inahitimisha kwa kusema kwamba muziki wa bongofleva umekuwa na wafuasi na wapenzi wengi sana hivyo kuna haja kubwa ya wasanii kurekodi nyimbo zinazogusa dhamira nyingi ili kuwawezesha vijana na vizazi vijavyo kutafakari na kuchangia mawazo katika nyanja mbalimbali za kijamii,kisiasa na hata kiuchumi. Kujikita katika dhamira ya mapenzi pekee kunabadili taswira ya muziki wa bongofleva kwani baadhi ya watu wanauchukulia kama muziki usio na maadili kutokana na kujikita katika dhamira ya mapenzi.

**Marejeleo**

[1]- Chachage, S. (2002), Ndani ya Bongo, Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni, Idara ya Sosholojia, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

[2]- Furman, W. (2002). The emerging field of adolescent romantic relationships. Current Directions in Psychological Science 11(5), 177- 180

[3]- Jesseemurithii,.'' Itikadi katika Riwaya za Dunia Yao (2006) na Mhanga Nafsi Yangu (2013) za S. A. Mohamed." IOSR Journal Of Humanities And Social Science (IOSR-JHSS). vol. 23 no. 09, 2018, pp. 39-46

[4]- Jilala, H. (2008), "The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meaning and Messagea in New Generation Songs in Tanzania". M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam(Unpublished).

[5]- Mangesho, P. (2003), Global Cultural Trends, The Case of Hip-hop Music in Dar es Salaam, M.A Dissertation, University of Dar es salaam(Unpublished).

[6]- Omari, S. (2006), "Mitindo na Matumizi ya Lugha Katika Muziki wa Kizazi Kipya", Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vol 69, 73-93.

[7]- Sanga, T.J. (2011), "Taswira ya Mwanamke Katika Mashairi ya Wasanii wa Kike wa Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dodoma, (Haijachapishwa).

[8]- Suriano, M. (2007), "Mimi Msanii Kioo cha Jamii" Urban Youth Culture in Tanzania as seen through Bongo fleva and Hip hop, Swahili Forum vol14. Pp 207-223.

**Diskografia**

**[1]-** Lavalava, (2018). Tuachane. Dar es Salaam: Wasafi Records Production.

[2]- Rayvanny, (2021). Kiuno. Dar es Salaam: Wasafi Records Production.

[3]- Mbosso, (2021). Baikoko. Dar es Salaam: Wasafi Records Production.

[4]- Roma, (2018). Zimbabwe. Dar es salaam: Tongwe Records Production

[5]- Kala Jeremiah, (2015). Nchi ya ahadi. Dar es Salaam Plexity records

[6]- Mrisho Mpoto ft Felly Kano, (2015). Waite. Dar es salaam: Soround Sound Studio

[7]- Ali Kiba, (2021). Infidèle. Dar es Salaam: Kings Music Records

[8]- Rayvanny, (2020). Ex-boyfriend. Dar es Salaam: Wasafi Records Production

[9]- Ali Kiba, (2020). Dodo. Dar es Salaam: Kings Music Records